AUTI ZA
ASOMAJI

ASTWEEK Sanduku
La Posta 87270
ombasa KENYA

LAMIC ENTRE

LIKUJENGA kituo cha
c Centre sisi wananchi
wa Pwani kusaidiwa
ngo na Mtukufu Rais Moi
utoa shillingi elfu ishirini
rikali ya Saudi Arabia
zaidi ya shillingi laki
na nusu.

o cha Islamic Centre si
i, ni kituo cha mikutano
michezo au maonyesho
mbali.

ni kama pana sababu
kumlaumu Mayor Rajab
kwa kuwapeleka
ni wa taifa letu kutoka
pia kuonesha michezo
a kitamaduni huko.

na mama wa Islamic
e wametenda mabaya na
u yao kuomba msamaha
Mayor wetu mpendwa
Sumba.

a Juma Majengo,
MBASA.

UWACHAGUE ONGOZI

NGOZI wa Islamic
e hao waliofanya kishindo
wenda kwa P.C. kupinga
ya Mayor Rajab Sumba
kuchaguliwa kwa kura
kututumikia Waisilamu.

mejipatia vyeo vyao tu
wenyewe na sisi
lamu wa Mombasa
a imani nao-kwa tendo

kki yetu twataka
gozi wa Islamic Centre
we kura na wala Islamic
e isiwe ya kundi au
hi ya watu tu.

tukubali baadhi ya kundi
ombasa Women Institute
asibu kuwa Islamic
re ni yao pekee.

ja Salimu,
E.

Tufuate maongozi ya Nyayo asema Galgalo Pwani

na KENYA NEWS AGENCY

MKUU wa Mkoa wa Pwani Bwana Luka Galgalo ametoa mwito kwa wananchi wa Pwani kuwa chonjo katika kutekeleza maongozi wa Nyayo ya Rais Moi.

Akihutubia mkutano wa kuadhimisha sherehe za Kenyatta Day Mombasa, Bwana Galgalo aliwakumbusha wananchi wa Kenya jinsi juhudi za ukombozi wa taifa hili zilivyofaulu kwa kujitolea na maongozi ya marehemu aliyeanzilisha taifa hili Mzee Jomo Kenyatta.

Akihutubia sherehe hizo Naibu Waziri wa Biashara Shariff Nassir alisema Wakenya wote wanathamini juhudi kubwa zilizofanywa na wale waliopigania uhuru wa taifa hili.

Sherehe hizo zilizofanywa katika kiwanja cha manispaa ya Mombasa zilihudhuriwa na ummati mkubwa wa wananchi wa tabaka zote za maisha.

Mkuu wa Mkoa hapo kwanza alisoma hutuba ya Rais kwa wananchi wa Pwani.

KWA UFUPI

MADAKITARI bandia wanaosemekana wanazurura wakiwadunga sindano wagonjwa katika lokesheni Ruruma Wilayani Kilifi wameonywa vikali wakome mara moja ama sivyo watashitakiwa na kupatiwa adhabu kali.

Onyo hilo limetolewa na Chief wa sehemu hiyo Bwana Victor Gamimba.

Alisema watu kadha wamefariki kutokana na tatizo hilo la hatari.

MWENYEKETI wa Chama cha Michezo Kenya Professa Ongeri amewaomba wanariadha humu nchini kuzidi kuhifadhi sifa ya michezo na kujitolea kwa taifa lao katika shughuli hizo.

Professa Ongeri alisema hayo Mombasa wakati wa kutoa vikombe kwa washindi wa matembezi wa Km. 20 wakati wa kuadhimisha Kenyatta Day.

ENZI YA NYAYO

KIPINDI cha "Enzi ya Nyayo" kilichotangazwa kwa muda wa saa nzima mnamo tarehe 20/10/80 kwa ajili ya kueleza mafanikio yanayopatikana chini ya uwongoziwa busara wa Mtukufu Rais Moi kilikuwa cha kuvutia na kuelimisha sana.

Kipindi hicho kilikuwa kwa mtindo wa mashairi yaliyopokewa katika Sauti ya Kenya, Stesheni ya Mombasa.

Mtayarishi wa Kipindi hicho, Bw Faraj Dumila anawashukuru pia wote waliokifanya kipindi hicho kifaulu.

Zaidi anamshukuru Mkuu wa Vipindi vya "National Service" Bw Jagi Ireri kwa mpango mwema wa kukifanya kipindi hicho kisikiwe vizuri na mara mbili.

Pia Bw. Dumila anaishukuru sana shule ya Coast Girls High School, hasa Mwalimu Khadija Bunu aliyewatayarisha wanafunzi wawili, Fatma Mohemed Ummeya na Sauda Saidi katika usomaji wa mashairi hayo.

Usomaji wao uliwavutia sana wasikilizaji.

Hivi sasa Bw. Dumila yuko katika shughuli ya kutayarisha mashairi ya Jamhuri kwa hivyo anawaomba washairi wajiweke tayari mapema.

WACHEZAJI WA ngoma za Kitamaduni kutoka Ethiopia wakati wakimtumbuiza Mtukufu Rais Moi siku ya nne ya Maonyesho ya Kilimo ya Nairobi ya mwaka huu. PICHA: KENYA NEWS AGENCY

UMOJA WA Lions Club Pwani, hivi juzi waliwapa watoto wa Port Reitz vyakula na vinywaji kuadhimisha mwaka wa wasiojiweza. PICHA: NATIONAL STUDIO

KATIKA SHEREHE ya kufana sana Mkuu wa Mkoa Bw. Luka Galgalo (mwenye suti nyeupe) anaonekana akitungua rasmi sehemu ya 'Coral Grill' ya Hotel ya Oceanic Mombasa. Katika picha (kushoto) Mayor wa Mombasa, Diwani Rajab Sumba na Bi Galgalo. PICHA: NATIONAL STUDIO

TWAMUUNGA MKONO MAYOR WETU SUMBA

MZOZO WA Islamic Centre Mombasa ulioletwa na baadhi ya viongozi wanaosimamia kituo hicho ni jambo ambalo halikuwa la busara na ni la aibu. Mtukufu Mayor wetu wa Mombasa Rajab Sumba, ndiye mlinzi, baba, kiongozi na msimamizi wa yote ya watu wa Mombasa bila kujadili dini au kabila.

Ni kiongozi aliyetoa na anayetoa uwongozi thabiti na mpenda amani, mpendwa na wote na hana dosari katika maongozi yake. Lilikuwa jambo baya, na hatua isiyofaa kwa akina mama wachache wanaojiwakilisha nafsi zao tu kwenda polisi na hata kufika kwa mkuu wa Mkoa kudai kwamba Mayor aliingia katika jumba la Islamic Centre bila idhini au kufuata taratibu na kanuni za kituo hicho.

Sisi tunapinga vikali hatua hiyo na kwamba tunamuunga kikamilifu Mayor wetu wa Mombasa Diwani Rajab Sumba, kwani hatua aliyoichukua ilikuwa na yaamana sana hasa kwa vile wageni wetu wa Kenya kutoka Ethiopia walikuwa hapo na ingekuwa jambo la aibu si kwa Mombasa tu, bali kwa taifa zima.

Kituo cha Islamic Centre si Msikiti, na ikiwa ni Usilamu hapana anayefahamu kanuni za Uisilamu kushinda Kadhi Mkuu wa Kenya Sheikh Abdulla Saleh Farsy ambaye Mayor wa Mombasa alishauriana naye kabla. Na kwamba Mayor alipata idhini kamili kutokana na msimamizi anayetambulikana wa kituo hicho.

Hatua hiyo haikuwa hatua ya busara, haikuwa hatua ya Kiungwana, kwani jambo hilo ni la umma wa Kiislamu na kwamba hapakutokea kitendo cha kuukashifu Uisilamu. Ikiwa ngoma hupingwa ngoma za taarabu za matusi mabaya sana, na mke na mume kuwekwa kati ya wanawake watupu. Jee huo ndio Uisilamu?

Kituo cha Islamic Centre kina mengi matatizo na ni juu ya Kadhi Mkuu wa Kenya na wanaohusika kuitafuta Halmashauri itakayoweza kuhifadhi kazi zinazohitajika katika kituo hicho cha taifa. Vitendo vilivyopitishwa na akina mama wachache wa Mombasa Women Institute wanaojinasibu kuwa kumiliki kituo cha Islamic Centre dhidi ya Mayor wa Mombasa ambaye ni mmoja kati ya watu waliojenga kituo hicho ni fedheha kwa wananchi wote wa Mombasa.

Matendo yao ni yao pekee na wala wasihusishwe na wengine kwa hali yo yote ile, kwani wenye hatia ni wale waliofanya makosa na haitakuwa jambo la busara kuwataja watu wa kabila maalumu na kuigiza samaki mmoja akioza wote huwa wameoza.

Twampongeza Mwenyekiti wa Kanu Shariff Nassir ambaye pia ni Naibu Waziri wa Biashara kupendekeza kuuzulu kwa maafisa 2 wa Mombasa Women Institute au kumchagua kwa kura mwenyekiti mwengine wa Umoja huo. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe. Mayor Sumba ni ukuta wa Mombasa.

Coastweek ★★

SWAHILI CROSSWORD NO. 100

JEMBE
UNGA SAFI NO. 1

KWENDA KULIA:
1. Mfalme wa bahari
6. Sehemu ndogo ya maji
7. Hufuatana na zinduna
8. Si PM
10. Namna ya kutunza na kuwalea wanyama
14. Ila, isipokuwa
15. Ua dogo
17. Kuzama majini
18. Sehemu ya mmea

KWENDA CHINI:
1. Tambua, jua
2. Fisi
3. Namna ya kuingiza au kupaka
4. Medical Officer
5. Inadi, kero
9. Idara ya Afya kwa Kimombo
11. Sehemu muhimu mwilini mwa kiumbe
12. Atoa maziwa
13. Nchi katika Asia
16. Pamoja na

JINA

SANDUKU LA POSTA

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 98:

[1] Khalid Hilal Busaidy, Sanduku la Posta 198, Malindi,

[2] Firdaws Zein, Sanduku la Posta 90190, Mombasa,

[3] Julius Katana, Sanduku la Posta 25, Kaloleni, Giriama.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 98 —

KWENDA KULIA:

1. MERIKEBU, 6. ARI, 7. RUFIJI, 8. AHI, 9. MANUKATO, 11. OKA, 13. AU, 16. USIA, 17. DHARAU, 18. SI, 19. AKA.

KWENDA CHINI:

1. MARIMBA, 2. RUFANI, 3. KIJIKO, 4. BA, 5. UROHO, 8. ATASUA, 10. AKUA, 12. ZAMA, 14. UDI, 15. TAI.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 30.10.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.